

## **Maswali**

1. Waisraeli walisafiri kwenda wapi?
2. Nani alimwongozea Mungu Waisraeli?
3. Waisraeli walipiga kambi kwa mlima gani?
4. Mungu alisema nini itafanyika Waisraeli wakimtii?
5. Nini ingefanyika kwa mtu atakayeguza mlima?
6. Nini ilifanyika BWANA alipokuja kwa mlima wa Sinai?
7. Mungu alinena nani?
8. Musa aliandika wapi amri kumi?
9. Mbona Mungu alipeana amri kumi?
10. Mungu anataka tufanye nini?

## **Majibu**

1. Waisraeli walisafiri kwenda nchi waliyoahidiwa.
2. Musa alimwongozea Mungu Waisraeli.
3. Waisraeli walipiga kambi kando ya mlima wa Sinai.
4. Mungu alisema kwamba hawa watu wakimtii watakuwa taifa lake takatifu.
5. Mtu atakayeguza mlima angekufa.
6. BWANA alipokuja kwa mlima wa Sinai kulikuwa na ngurumo, umeme, wingu zito, sauti ya paragumu, moto na mtetemeko wa nchi.
7. Mungu alinena na Musa.
8. Musa aliandika amri kumi kwa mbao 2 za mawe.
9. Mungu aliwapa Waisraeli amri kumi ziwasaidie waishi maisha ya utawa.
10. Mungu anataka tumsujudie.

## **SHULE YA JUMAPILI YA CBM**

**Awamu ya 1 Mwaka wa 2**



## **3 Amri Kumi**

### **Marejeo**

Kutoka 19 na 20

### **Kiini cha somo**

1. Kuona vile Mungu alimpa Musa amri 10
2. Kujua amri 10 ni nini?
3. Tufikirie juu ya amri 10.

### **Maneno maalum**

1. Waisraeli waondoka Misri + nchi ya ahadi + Mungu alipeana + Mlima wa Sinai
2. Mungu alizungumza na Musa + wakitii watakuwa taifa langu + Tutatii.
3. Tayarisha + siku ya tatu + usiguze mlima
4. Dhoruba + BWANA akaja kwa moto + Mungu akaita Musa.
5. Amri 10 + mbao za mawe.
6. Kuishi kwa njia ya Mungu
7. Yesu anatufundisha tufikirie.
8. Abudu Mungu + ishi maisha ya utawa.

**3.1** Wana wa Israeli walianza safari wakitoka Misri. Waliongozwa na Musa kwenda nchi waliyoahidiwa na Mungu. Mara nydingi hawa watu walilalamika walipo kuwa na njaa au kiu. Lakini Mungu aliwapa walichotaka. Baada ya kusafiri kwa miezi 3, Waisraeli walifika kwa Mlima wa Sinai. Walipiga kambi jangwani mbele ya huo mlima.

**3.2** Musa alienda mlimani na akanena na Mungu. Mungu alisema, "Nimeokoa hawa watu kutoka Misri, wakiti sauti yangu na washike amri zangu watakuwa taifa langu takatifu."

Musa alirudi kwa watu na wakajibu, "Tutafanya lolote aliloamuru Mungu!" Musa akarudisha hilo jibu kwa Mungu.

**3.3** Mungu akamwambia Musa kwamba watu wawe tayari kuonana naye. Lazima watayarische mawazo yao na waoshe nguo zao. Mungu atateremka kutoka mlima wa Sinai siku ya tatu na kila mtu ataona. Lakini mtu yejote akiguza huo mlima atakufa.

**3.4** Watu walijitayarisha. Siku ya tatu kulikuwa na ngurumo na umeme. Mlima ulifunika kwa wingu zito na kukawa na sauti ya paragamu. Watu walismama chini ya mlima wakiwa na uwuoga. Mungu alishuka juu ya mlima katika moto. Nchi ilitetemeka. Sauti ikaendelea kuwa kubwa. Mungu aliita Musa na Haruni wakwee mlima. Mtu mwengine asikwee bure atakufa.



## AMRI

1. Mimi ni Bwana Mungu wako. Usiwe na miungu mingine ila mimi.
2. Usiabudu sanamu.
3. Uliheshimu jina la Bwana Mungu wako.
4. Ikumbuke siku ya Sabato na uitakase.

## KUMI

5. Waheshimu baba yako na mama yako.
6. Usiuwe
7. Usizini
8. Usiibe
9. Usiseme uongo
10. Usitamani vitu vya watu wengine

**3.5** Mungu akaambia Musa haya maneno. Tunaziita amri kumi. Musa akaziandika juu ya mbao za mawe.

**3.6** Mungu alimpa Musa amri zingine pia. Aliwapa ili ziwasaidie watu waishi pamoja kwa utawa.

**3.7** Yesu aliwafundisha wanafunzi wake wajue amri kumi zina maana gani kwao. Alisema, "Mliambiwa msiuwe. Lakini hata usikasirikie mwenzako." Ukipenda kitu kingine chochote zaidi ya Mungu, hicho kitu ni sanamu kwetu.

**3.8** Tuwe waangalifu sana juu ya amri kumi. Mungu anataka tumsujudie. Njia moja ya kufanya hivi ni kuishi maisha ya utawa.